

# **Bilal Funeral Services**

mada ya majadiliano ya leo, tarehe 05/09/2015

Leo tuta zungumzia mada zifuatazo. Mada hizi kwa kiasi kikubwa za eleza sheria na masharti za Bilal funeral services.

## **1. Ufafanuzi**

- 1.1. **Familia** – watu wanaoishi kwenye nyumba moja, Baba na Mama pamoja na watoto wanaoishi nao walioko chini ya dhamana yao.  
Mtoto akiowa au kuolewa atatoka katika dhamana ya wazee wake au wazee wanaomlea katika mchango huu.

## **2. Kwanini kamati ya maziko?**

- 2.1. Jamii ya africa mashariki imekuwa kubwa na kuna haja ya kujiunga kwenye shughuli za maziko
- 2.2. Hii ni kamati ya mwanzo ya africa mashariki inaozika kwa kufwata fiqh ya Ahlulbayt.
- 2.3. Kupanga mazishi kwa kutumia “bima” inayo weza kuendelea nakutufaidisha kwa miaka mengi inayofwata.

## **3. Michango**

- 3.1. Gharama za kuzika hapa UK ni kiasi £3500 - £5000 (makisio),
- 3.2. Michango ya Bilal kwa kila famili ni **£100** kwa kuanzia, hii itadhamini familia kwa muda wa **mwaka mmoja**.
- 3.3. Baada ya mwaka tangu mchango wa mwanzo, kila familia itawajibika itoe tena £100 za mwaka unaofuata, hii ikiwa jumuiya haikufanya maziko katika kipindi hicho cha mwaka.
- 3.4. Michango itaendelea hivi mpaka kila familia ichangie £400 au miaka 4, hii itawezekana ikiwa jumuiya ya Bilal haikufanya maziko katika kipindi hicho cha miaka 4.
- 3.5. Baada ya hapo kamati ya maziko itakaa na kuamua mambo mawili:-
  - 3.5.1. kusimamisha michango kwa mwaka unaofuata, au
  - 3.5.2. kupunguza kiasi ya michango kwa kila familia.
- 3.6. Familia inayojiunga baada ya michango kwishakuanza kwa muda wa mwaka au zaidi, hiyo familia itahisabiwa tarehe ilojiunga na itabidi ikamilishe miaka 4 kwanza kabla hajapata faida ya kusimamishiwa au kupunguziwa katika mchango wake.

## **4. Jee pindipo jumuiya ikifanya maziko?**

- 4.1. Ikiwa jumuiya (kwa masikitiko) imefanya maziko:
  - 4.1.1. Kila familia itatakiwa ilipe £100 ndani ya mwezi mmoja tangu maziko kumalizika, familia ya marehemu muda utazidi mpaka miezi mitatu
  - 4.1.2. Mwaka huu hautoingia katika ile miaka 4 ya kusimamisha au kupunguziwa mchango.
  - 4.1.3. Ikiwa marehemu kaacha usia kwa familia yake, au familia imeamua walipe gharama zote za maziko, ule mda wa miaka 4 hautoadhirika.

4.2. Swali:

4.2.1. **Tanbihi** - Wengine wanaweza kusema, si tayari tushailipa £100? Kwanini tena isiingizwe kwenye kile kipindi cha miaka 4?

4.2.2. **Jawabu:** hii ni njia ya kujieka sisi wenyewe pindipo tukitokewa na dharura ya vifo vingi kwa pamoja (kama nduguzetu wa Barking sasa hivi).

4.3. Familia inayotoa mchango haitolazimika kulipa gharama za maziko, wakiamua kulipa pesa zitaingia kwenye mfuko wa maziko kama tulivyoeleza kabla.

4.4. **Mchango wa mwaka ambao umetolewa hauwezi kurejeshwa.** Ukiamua kujitoa au kutoendelea na Bilal Funeral Services, itabidi mwaka unaofuata usiendelee na mchango tena.

## 5. Mipangilio ya maziko

5.1. Kukitokea kifo, utatakiwa uifahamishe kamati ya Bilal moja kwa moja.

5.2. Bilal itashughulikia kutoa maiti kutoka hospitali

5.3. Bilal itashughulikia kuosha maiti, kuswalia maiti na kuzika (Garden of Peace).

5.4. Fiqh ya Ahluylbayt

5.5. Mwanachama akifa nje ya nchi UK, Bilal ita saidia (itachangia) kifedha peke tu.

Nime soma na kufahamu mada zilizo humu. Sharia na masharti uta zipata katika website: [www.bilaleducation.org/downloads](http://www.bilaleducation.org/downloads)

NAME and SIGNATURE